

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

SHULE YA SEKONDARI SIGILI

S.L.P 656

NZEGA

0759296609/07548014

KUMB Na.SSS/F1/2021

Jina la Mwanafunzi

Shule ya Msingi Aliyosoma

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SIGILI WILAYA YA
NZEGA MKOA WA TABORA MWAKA 2021**

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Mwamala mwaka 2021. Shule ya Sekondari Sigili ipo umbali wa kilomita 158 Kasikazini Magharibi mwa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**, Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na Mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku nane. Mwanafunzi atakayechelewa kuripoti kwa makusudi hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Mzazi wake/Mlezi wake.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

**2.1 Sare za shule
Wavulana**

Sare za shule hii ni suruali yenye marinda mawili kila upande na isiyobana (rangi ya Nyeusi).Shati jeupe lenye mikono mifupi.T-shirt rangi ya Bluu yenye nembo ya shule ambayo mwanafunzi atavaa mara mbili kwa wiki kama Sare ya Shule.Viatu vyeusi vya kufunga na jidamu(kamba).Soksi nyeusi ndefu.

Wasichana

Sketi ndefu yenye marinda (rangi Nyeusi) ndefu yenye kuvuka magoti na kufunika saluta za miguu. Shati jeupe lenye mikono mifupi.T – shirt rangi ya Bluu yenye nembo ya shule ambalo mwanafunzi atavaa mara mbili kwa wiki kama Sare ya Shule.Viatu vyeusi vya kufunga na jidamu(kamba).Soksi nyeupe ndefu. Hijabu ivaliwe na sketi kwani suruali hairuhusiwi.

SARE ZA MICHEZO

Wavulana - T-shirt ya Bluu yenye nembo ya shule, Bukta ya bluu na raba

Wasichana -T-shirt ya Bluu yenye nembo ya shule, suruali ya track suit rangi ya bluu,raba.

2.2. Daftari Tisa (9) kubwa(Counter Books Quire Two),Kalamu na Mkebe wa hesabu(mathematical set).

2.2 Matibabu ya Mwanafunzi ni juu ya mzazi/mlezi.

2.3 Chakula cha mchana kwa mwanafunzi ni juu ya mzazi/mlezi

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995.

Aidha, ina zingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:-

- (a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Viongozi wa wanafunzi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kushiriki kikamilifu kufanya kazi za jioni.
- (d) Kuwahi kufika shule ni jambo la lazima.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- (g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- (i) Kutunza mali za umma

4.0 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

(a) Wizi

(b) Uasherati na Ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi

na kadhalika

(e) kupigana au kupiga

(f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma

(g) Kudharau Bendera ya Taifa

(h) Kuwa mjamzito / kupata mimba

(i) Kuoau au kuolewa

(j) Kutoa mimba

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa

shule au watu

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi

(m) Kuwa na simu ya mkononi

5.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na Mwanafunzi.

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

5.1 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
REGINA AMOS DODo
MKUU WA SHULE

THE UNITED REBUPLIC OF TANZANIA

SIGILI SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by medical officer)

Pupils full Name.....

Age.....Year.....Sex.....

Stool Examination.....

Urine/Pregnancy Examination.....

Blood counted (red and white).....

Syphilis Text.....

Chest test.....

Spleen.....

Addition in formation leg physical defects/ impairment + or chronic disease
requiring special Treatment

.....
.....

I certify the above Examined students is **OKEY/ NOT OKEY** or / recommended / **HIS / HER** secondary Education.

Signed.....

Designation.....

Official stamp.....

Date.....

Delete whichever is inapplicable